KUIMARISHA KANISA LAKO

# KUWA KANISA LENYE MATOKEO!

MWONGOZO KWA VIONGOZI WA WARSHA

## Maelezo

Warsha ya kuimarisha Kanisa lako huwawezesha Viongozi wa Kanisa kuliweka kusanyiko kwenye lengo la kazi yake kama wakala wa Mungu katika eneo husika. Warsha inatoa umuhimu wa maono yanayoelezeka kibiblia, inawaongoza kwenye tabia kumi za Kanisa lenye afya, na inawavuta Viongozi kuliona Kanisa lao kama mfumo unaoweza kuwa na matokeo muhimu katika jamii yake.

Mtandao wa Kuzidisha
Makanisa Mengi Zaidi, Makanisa Yenye Nguvu

## MWONGOZO WA KIONGOZI |

Warsha ya kuimarisha kanisa lako huwezesha viongozi wa kanisa kuliendeleza kusanyiko katika lengo juu ya kazi yake, kama wakala wa Mungu wa mahali Fulani linapoungana na Mungu katika utendaji wake. Warsha hutoa umuhimu wa maono yanayoelezeka kibiblia, humtambulisha kiongozi kwenye tabia kumi za kanisa lenye afya, na huwaalika viongozi kuliona kanisa lao kama mfumo unaoweza kuwa na matokeo muhimu juu ya jamii yake.

Kitabu hiki kinatoa maelekezo na mashauri ya nyongeza kwa watu wanaotarajia kuongoza warsha kanisani mwao au kwenye makanisa mengine. Kama unahitaji msaada wa kuongoza warsha tafadhali wasiliana na mmoja wa wawakilishi wa mtandao wa kuzidisha nchini mwako (orodha inapatikana katika mtandao wetu). Mtandao wetu pia tunatoa matukio mawili ya upandaji wa kanisa. Kupanda makanisa yenye afya na faragha ya mpanda kanisa. Unaweza kupata taarifa zaidi kupitia mtandao wetu ama mwakilishi wa mtandao wetu.

Vifaa kwa ajili ya viongozi wa warsha:
1. Kitabu cha Kiongozi
2. Kitabu cha Mshiriki
3. Slaidi (zinazopatikana kwenye CD au mtandao wetu
4. Msaada kutoka kwa mkufunzi wa ukuaji mkamilifu wa kanisa (tembelea mtandao wetu: www.multiplicationnetwork.org)

## JINSI YA KUTUMIA MWONGOZO HUU |

Mwongozo huu utakusaidia kuwaongoza washiriki katika warsha yote. Kila ukurasa unaonesha kinachoonekana kwenye mwongozo wa mshiriki katika sehemu kuu ya ukurasa na taarifa kwa viongozi iliyo pembezoni au yenye herufi nyembamba zilizokolezwa mno katika kitabu kile kile. Majibu kwa ajili ya kitabu cha washiriki yanapatikana kwenye mwongozo huu katika kurasa za washiriki zenye herufi kubwa, zimepigiwa mistari, na kukolezwa (mf. **MUNGU**).

Kwa kila kijarida, kitabu kinatoa maswali ambayo washiriki watayajibu wawili wawili au kwa vikundi vidogo kadri muda unavyoruhusu. Hapatakuwa na muda wa kutosha kwa washiriki kujadili maswali yote kwa kila kipindi, hivyo tunawatia moyo wakufunzi kuchagua yale yanayofaa zaidi ili washiriki wayafanye vizuri. Tunamhamasisha kila mkufunzi kuyaboresha zaidi mafundisho haya kwa kutumia uzoefu, mafafanuzi na mifano yake.

## RATIBA ILIYOPENDEKEZWA |

Tumependekeza ratiba ya warsha ya siku moja. Hata hivyo tunakutia moyo kupanga ratiba kulingana na kile kinachofanikiwa kwako na kwa washiriki wako. Unaweza pia kuifanya warsha kwa zaidi ya majuma manne (kipindi kimoja kwa kila juma) au siku ya Ijumaa jioni na Jumamosi asubuhi ili kupunguza gharama.

Kila kipindi kimeandaliwa kudumu kwa saa moja na nusu. Tafadhali acha muda wa kutosha mwishoni kwa ajili ya washiriki kujaza fomu ya tathmini.

Ikiwezekana chukua picha ya warsha yako na uitume kwenye mtandao wa kuzidisha pamoja na taarifa yako ya tukio (angalia mtandao wetu kwa ajili ya fomu ya ripoti au ukurasa wa 31 wa kitabu hiki kwa taarifa zaidi ambazo tungependa ututumie.

## VIFAA VYA WARSHA |

Lengo letu ni kuifanya warsha iwafikie viongozi wengi iwezekanavyo kwa gharama nafuu ama pasipo gharama. Unaweza kutoa nakala za kitabu cha mshiriki na kukitumia kwenye makanisa yaliyo husika kuandaa vyakula na viburudisho.

Jisikie huru kuunda sura tofauti ya juu ya kitabu mtindo unaofaa zaidi kwenye mazingira ambayo kitabu kitatumiwa.

**Mtandao wa kuzidisha**
Rejea zote za kibiblia zimetolewa kutoka Toleo Jipya la Kimataifa (New International Version, Copyright 1973,1978, 1984)

## YALIYOMO

**Kipindi cha 1 |**
Shauku, Maono,Dhamira ........ 3

**Kipindi cha 2 |**
Ishara tano za Kanisa Lenye Afya ........ 7

**Kipindi cha 3 |**
Kazi Tano za Kanisa Lenye Afya ........ 15

**Kipindi cha 4 |**
Mfumo wa mabadiliko ........ 24

**Kiambatanisho|**
Misingi ya Kitheolojia ........ 31

**Fomu ya tathimini |** ........ 33

**Cheti |** ........ 35

| RATIBA INAYOPENDEKEZWA | |
|---|---|
| Usajili na ukaribisho | |
| Muda wa Ibada | DAKIKA 30 |
| **KIPINDI CHA 1** | DAKIKA 60 |
| **KIPINDI CHA 2** | DAKIKA 60 |
| Pumziko | |
| **KIPINDI CHA 3** | DAKIKA 60 |
| **KIPINDI CHA 4** | DAKIKA 60 |
| Kipindi cha maswali na majibu, tathimini, kufunga | |

KIPINDI CHA 1

# SHAUKU, MAONO, DHAMIRA




## "UKUAJI MKAMILIFU WA KANISA NI NINI?

Ukuaji wa Kanisa unakuwa wa afya pale tu unapoinua maendeleo kwa viwango vyote vya maisha ya Kanisa, siyo tu ongezeko la idadi ya washirika au wahudhuriaji. Kanisa lenye afya linajiona lenyewe kwa mjengo mpana wa makusudi ya Mungu kwa ulimwengu, ubinadamu na kwa mataifa yote – kufanywa upya kwa viwango vya maisha. Kanisa linachukua utawala wa Mungu kama hatua ya msingi na hutafuta kuupanua katika maeneo yote ya maisha (nyumbani, katika jamii, kazini nk) kupitia matokeo ya habari njema za Yesu Kristo.

## MUUNDO WA UKUAJI MKAMILIFU WA KANISA

Kipindi hiki hutusaidia kukumbuka kuwa uhusiano wetu wa kiibada na Mungu ni wa lazima ili tuweze kutimiza kazi aliyotuita kuifanya. Tunapokuwa na shauku na kazi ya Mungu, tunafanya maono ya kile ambacho Mungu anataka kufanya na anachoweza kufanya kupitia kwetu. Tunapoitikia wito wa Mungu kwa utii, Kanisa linatoka nje na kutimiza utume kwa ulimwengu. Hii inatokea pale tu tunapoelewa kile ambacho Biblia inatufundisha kuhusu uhusiano kati ya Mungu, Kanisa na jamii yetu.

**Zoezi**| Unganisha Nukta

Jaribu kuunganisha pointi/nukta zote kwa kuchora mistari minne, lakini pasipo kuinua penseli yako.



Mara nyingi watu hustaajabu kuona kwamba ili mtu ashughulikie tatizo anahitaji kuchora mistari inayopitiliza pale alama (doti) zilipo. Kuna nyakati tunahitaji kupanua namna yetu ya kufikiri "kufikiri nje ya sanduku" – ili tuwe waaminifu kwa Mungu. Ni muhimu kutambua kuwa sote tuna "alama" (doti) za kiakili na falsafa za huduma zinazoweza kutuzuia kuwa waaminifu kwa misheni yetu na kuona matokeo bora kutoka kwenye huduma zetu.

Kipindi hiki kinaanza na maelezo ya kukua kwa kanisa lenye afya.

**"Mkate upande mmoja na maziwa kwa upande mwingine" |** Elezea umuhimu wa kutumia mbinu na mikakati ya ukuaji wa kanisa kulingana na mazingira (muktadha).

Miaka iliyopita masoko makubwa ya vitu huko Marekani waligundua mbinu za kuwafanya watu kununua bidhaa zaidi. Watu walifika sokoni kwa kusudi la kupata kitu fulani cha msingi, kwa mfano mkate na maziwa, lakini wangenunua zaidi ikiwa wangepitia kwenye bidhaa na makabati fulani yenye ofa maalum. Siku hizi watu wa masoko wanasomea mbinu nyingi ili kupata mbinu za kuwafanya watu wanunue zaidi wanapokuwa sokoni, kutokana na aina ya muziki wanazopiga (muziki wa polepole) namna wanavyoweka bidhaa zao (kuweka bidhaa wanazotaka kuuza zaidi kwenye usawa wa upeo wa macho ya mteja).

Ikiwa watu wa masoko wanajifunza sana jinsi watu wanavyonunua ili tu waweze kuuza bidhaa zaidi, je, kwa nini sisi kama wakristo tusijifunze vile tuwezavyo kwa habari za watu na tabia zao ili tuweze kuwaalika kwa ufanisi kumjua Kristo na wawe sehemu ya watu wake? Pamoja na kuwa ujumbe wa msingi wa uzima katika Kristo kamwe hautabadilika, tamaduni na namna za watu kutenda mambo hubadilika. Kwa hiyo mbinu na mikakati ya kushirikisha injili itahitaji kubadilika ili kuendana na muktadha ambao tunamhubiri Kristo.

**Maono |** Lengo kuu ni kwamba viongozi waelewe umuhimu wa kuwa na maono ya Kibiblia, yaliyo wazi na yenye mvuto yanayowasukuma wengine kuungana na Mungu katika kile anachokifanya katika maeneo yao.

**Kazi ya Miwani |** Jamaa ambaye alihitaji miwani alishangaa sana pale alipoivaa kwa mara ya kwanza na akagundua kuwa aliweza kuona vizuri zaidi. Tunapoyaona mambo kwa kupitia maandiko (sisi wenyewe, hali zetu za maisha na majirani zetu), tunayaona mambo kwa uwazi zaidi. Tunaanza kuwa na mtazamo wa Ki –Mungu juu ya maisha yetu na jamii zetu.

**Mifano ya Kibiblia |** Kanisa lisipokuwa na maono yanayoelezeka Kibiblia mara huwa chama cha jamii, ama mkahawa wa kiroho wa chakula cha haraka, mahali ambapo tunakuja kupata tunachokitaka. Badala yake kuwa mwaminifu kwa Mungu, tunahitaji kuyaandaa maisha yetu kama Kanisa kwa kile Yesu anachokisema kuwa sisi ni watu gani. Tunahitaji kuliangalia kusanyiko letu na jamii yetu kwa kupitia macho ya Bwana Je, Mungu anatuita tuweje na tufanye nini?

**Mfano wa Wajenzi |** Mara Yule mtu aliwakaribia watu waliokuwa wakivunja mawe na akawauliza walikuwa wanafanya nini. Wa kwanza akasema "tunatafuta maisha". Wa pili akasema "Nafanya kazi yangu kama mvunja mawe". Wa tatu akasema "Ninajenga kanisa kuu zuri zaidi ya yaliyowahi kuonekana katika mji huu". Mara nyingi katika kanisa tunafanya kazi zetu tukifikiri tu kuhusu shughuli ya muda mfupi – kuandaa somo la shule ya Jumapili, kupeleka chakula kwa familia zenye uhitaji, kuweka sadaka zetu kwenye chombo cha sadaka – pasipo kuona maono makubwa aliyo nayo Mungu kwa ajili ya kazi, maisha, familia na jamii iliyobadilika kupitia Habari Njema za Yesu Kristo.

## MAONO

Kuwa na maono ni kuiangalia <u>**HATIMA**</u> na kuona kile ambacho Mungu anatakakutendakupitiakwakoilikufanikishamakusudiyakeyaukombozi..

- Kazi ya miwani.
- Mifano ya Kibiblia: Maandiko yana mifano mingi ya viongozi wenye maono ya kile alichotaka kufanya Mungu ndani yao na kupitia kwao.
  1. Abraham kuwa na uzao mwingi, nchi kwa ajili yao na kuwa Baraka kwa ulimwengu. Mwa. 12:1-3.
  2. Nuhu Kutunza salama familia yake na wanyama katika gharika. Mwa. 6:13-14, 17-20.
  3. Yoshua na Kalebu kuingia katika nchi ambayo Mungu aliwaahidia waisraeli. Hes. 14:6-9.
  4. Paulo kuwapelekea injili mataifa katika Dola yote ya Rumi. Mdo. 26:13-18.
  5. Yesu kuleta uponyaji, tumaini na uhuru.Lk. 4:18-19
- Kanisa lenye afya huanza na maono yenye motisha na yaliyo wazi.
- Mfano wa wajenzi.

***Je, ungependa kuwa mshiriki wa kazi ya kuujenga ufalme wa Mungu? Je, ni lipi utaweka jiwe la kwanza?***

> *"Na pasipo imani haiwezekani kumpendeza,kwa kuwa kila amwendeaye yeye lazima aamini kuwa yeye yuko,na huwapa thawabu wale wamtafutao"* Ebr. 11:6
>
> *"Mna hila nyingi mioyoni mwa watu,bali shauri la BWANA ndilo litakalosimama"* Mith. 19:21

**Mchoro |** Uhusiano kati ya Mungu – Kanisa – Jamii




Sehemu hii huelezea mahusiano kati ya Mungu, Kanisa na Jamii yake katika namna ya utaratibu. Unapowaongoza washiriki katika sehemu hii, tumia mifano na simulizi kutokana na huduma yako binafsi ili kufafanua kila pointi inayotolewa.

Washiriki wasome mistari ya ufunguo inayohusika na uhusiano wa kanisa na Mungu. Uhusiano huu ni ufunguo kwa kanisa kudumisha utambulisho wake, maono na shauku yake. Uzima wetu unatoka kwa Mungu. Tusipomtegemea yeye, kamwe hatuwezi kutimiliza dhamira yetu. Wainjilisti wakuu, wachungaji na wapanda kanisa ni wakuu kwa sababu wanatunza uhusiano wao na Mungu. Kutumia muda pamoja na Mungu kupitia maombi na kutafakari maandiko, ni muhimu kwa ajili yetu kumjua Yeye, kujua mapenzi yake na kuwa na nguvu za kumtumikia.

Mchoro unatoa mahusiano ya aina tatu ndani ya picha moja.:

**1. Uhusiano kati ya Kanisa na Mungu**

**KANUNI |** Ili kusanyiko/Kanisa lolote liguse jamii yake, hakuna kilicho muhimu kama uhusiano udumuo wa kina pamoja na Bwana.

> *"Mimi .ndimi mzabibu, ninyi ni matawi. Mtu akikaa ndani yangu ,nami ndani yake,huyo huzaa sana;maana pasipo mimi ninyi hamwezi neno lolote."* Yohana. 15:5
>
> *"Bwana asipoijenga nyumba,aijengaye afanya kazi bure"* Zab. 127:1

**2. Uhusiano kati ya Mungu na Jamii**

**KANUNI |** MFANO WA YESU KUVAA MWILI, Wafilipi 2:5-8
Wakati wote Mungu yuko kazini katikati yetu. Yuko pale tulipo siku nyingi kabla ya mwinjilisti au mmisionari wa kwanza hajafika.

> *"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu,hata akamtoa Mwanaye pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee,bali awe na uzima wa milele"* Yohana. 3:16
>
> *"Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji na vijiji,akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina"* Mathayo 9:35
>
> *"Na alipowaona makutano aliwahurumia..."* Mathayo 9:36

**3. Uhusiano kati ya Kusanyiko /Kanisa na Jamii**

**KANUNI |** Mungu anataka kutenda kazi kupitia kwetu (sisi). Sisi ni mikono na miguu yake na sauti yake katika ulimwengu huu. Kabla ya kufanikiwa katika makubwa, lazima tuwe waaminifu kwa mambo madogo.

> *"Yesu akamwambia Baba yake,"Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni,nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni."* Yn. 17:18

Soma mistari inayoongelea uhusiano kati ya Mungu na jamii. Mungu ana mzigo na waliopotea. Katika huduma ya Yesu, aliwaendea waliopotea, na waliotengwa na jamii ili kuwaponya na kuwarejesha upya.

Mungu pia anashughulika na mioyo ya watu na jamii kabla sisi hatujafika mahali pale. Anatuita tushiriki katika kile anachokifanya, na anatenda kazi kupitia kwetu tunapowafikia watu kwa Injili.

Mwisho, soma mistari inayoongelea uhusiano wa kanisa na jamii yake. Mungu anatuita tuwe mikono yake, miguu na sauti yake katika jamii aliotuweka. Mwombe mtu atoe mfano wa kanisa analolijua ambalo linatunza uhusiano wake na Mungu na pia ambalo ni mikono ya Mungu na miguu katika jamii yake.

**Kisa cha Florence Chadwick | Asubuhi ya mwezi Julai 4, 1952, Florence Chadwick alizamia kwenye maji ya baridi katika kisiwa cha Katalina katika jaribio la kuogelea kuelekea pwani ya California umbali wa maili 22. Alikuwa amekwisha vuka mifereji mbalimbali, mito na maziwa, lakini siku hii mambo yalikuwa tofauti. Maji yalikuwa ya baridi sana na ukungu haukumruhusu kuona mbali zaidi. Baada ya dakika 15 za kuogelea, Florence alikuwa amechoka, na akawaomba watu wa mashua. Mama yake na mkufunzi wake walijaribu kumsaidia aendelee kuogelea, lakini baada ya dakika chake alikata tamaa, akashindwa kufikia lengo lake. Mashua ilipofika pwani, akagundua kwamba alikuwa amebakiza mita 700 tu kutoka pwani wakati alipojiondoa. Katika hali ya kufadhaika, Florence alieleza kwamba kama angeliweza kuiona pwani angeweza kufika licha ya baridi na kuishiwa nguvu, lakini ukungu ulimzuia kuona. Miezi kadhaa iliyofuata Florence alirudi kisiwa cha Katalina na akathubutu tena tendo la ujasiri. Maji ya baridi na ukungu ulikuwa ule ule, ama unaozidi jaribio lake la kwanza, lakini aliogelea hadi pwani ya California. Alipoulizwa aliwezaje kufanikiwa , alijibu "wakati huu pwani ilikuwa tayari imo ndani ya moyo wangu".**

**Swali kwetu sisi kama viongozi wa Kikristo ni lile lile, Je, tuna maono ya MUNGU ndani ya mioyo yetu kwa ajili ya jamii zetu? Je, tuko tayari kupambana na upepo na mawimbi ili kuweza kufanikisha makusudi ambayo Mungu anayo kwa ajili yetu?**

*"Roho wa Bwana yu juu yangu kwa kuwa amenitia mafuta kuwahubiri maskini Habari njema. Amenituma kuwatangazia mateka habari za kufunguliwa kwao na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa; kutangaza mwaka wa Bwana uliokubalika."* Luka 4:18-19

*"Bwana wake akamwambia ,Vema mtumwa mwema na mwaminifu! Ulikuwa mwaminifu kwa madogo;nitakuweka juu ya mengi. Ingia katika furaha ya Bwana wako."* Mt. 25:21

**Mchoro** | Shauku, Maono, Dhamira




Sehemu hii inazungumzia dhana kupitia mchoro unaotoa muhtasari wa dhamira ya kanisa. Mchoro umeelezewa kwa njia ifuatayo:

1. Kwa sababu ya uhusiano wake na Mungu, kanisa lina SHAUKU ya kumtumikia Yeye. Jamii huona shauku hii ya vitendo ambayo husaidia kuwa USHUHUDA wa kanisa.
2. Mungu anatenda kazi katika jamii na kanisa linabeba MAONO kwa kuwa linaelewa kitu ambacho Mungu anafanya katika ulimwengu. Hii hulipatia kanisa hisia ya KUSUDI.
3. Mungu analituma kanisa lenye DHAMIRA kwenye jamii yake na huongeza BARAKA pale kanisa linapomtii Yeye.
4. Kila kitu kinazunguka msalaba na ujumbe wa Yesu Kristo.

Kanisa linapokuwa na uhusiano mzuri na Mungu, lina shauku kwa ajili ya Misheni ya Mungu. Kanisa linapoelewa mpango wa Mungu kwa ajili ya jamii, Kanisa lina maono. Basi Kanisa liko tayari kubeba miisheni yake kwa jami. Baraka za Mungu zinakuza Kanisa kwa kuwa linabeba ushuhuda kwa neno, kwa tendo kwenye jamii.

**Hitimisho:**

Hadithi ya Florence Chadwick, Julai 4, 1952, kisiwa cha Catalina.

**Changamoto:**

## *Kama sio leo, lini? Kama sio mimi, ni nani*

Swali kwa ajili yetu, kama viongozi wa Kikristo ni lile lile. Je, tuna maono ya Mungu kwa ajili ya jamii zetu ndani ya mioyo yetu? Je, tuko tayari kupambana na upepo na mawimbi ili kufanikisha makusudi aliyo nayo Mungu kwa ajili yetu?

KIPINDI CHA 2
# ISHARA TANO ZA KANISA LENYE AFYA.

**UTANGULIZI.**

Kipindi hiki kinatoa maelezo ya vidokezo vitano muhimu kwa Kanisa lenye afya:

1. Maono yaliyo wazi
2. Kuimarisha Uongozi.
3. Washirika waliohusishwa katika huduma
4. Uwakili wa rasilimali
5. Muunganiko kati ya andiko na muktadha

Kuelewa vidokezo hivi huwasaidia Viongozi kupanga kimkakati na kutathimini huduma zao.



**Mfano** | Mtu aliye juu ya njia ya reli.

Ili kuwa na Kanisa lenye afya na linalokua tunapaswa kuzingatia sehemu zote za maisha ya Kanisa na huduma (ishara tano na kazi tano)

**Diagram** | "Ishara zilizo hai za Kanisa lenye afya"




**Mtu akiwa juu ya njia ya reli|**
Kulikuwa na mtu ambaye siku moja alikwenda kutembea juu ya njia ya reli. Akahisi reli inaanza kutikisika chini, lakini hakuona treni (gari moshi) yoyote, hivyo akaendelea kutembea. Ndipo akasikia muungurumo wa treni kwa karibu sana, lakini hakuiona treni mbele yake, akaamua kuendelea kutembea. Ni nini kilitokea baadaye? (Aligongwa na treni, ambayo ilikuja nyuma yake). Mtu huyu alitegemea macho yake tu na hakujua treni ilikuwa inakuja nyuma yake. Kutokuzingatia ishara/ alama zinazotuzunguka kunaweza kuleta madhara makubwa!! Kwa njia hiyo hiyo ndani ya kusanyiko tunahitaji kuzifikiria alama zote za kitu kinachoendelea katika maisha ya kanisa, sio kipengele kimoja au viwili tu.

Pointi za kipindi cha 2 na cha 3 ni kwamba ili kuwa na kanisa lenye afya na linalokua, tunahitaji kukuza maeneo yote ya uhai wa kanisa. Vinginevyo kanisa kwa ujumla litapata shida.

**Maeneo ya kanisa lenye afya** | Ishara 5 katika kipindi cha 2 na kazi 5 katika kipindi cha 3 zinahusiana na zote ni muhimu kwa makanisa, haijalishi hatua za kusanyiko katika ukuaji/ukomavu ni zipi.

Baada ya maelezo ya kila ishara na kazi, kuna maelezo machache ambayo washiriki wanaweza ili kutathmini kanisa lao.

**Maono yaliyo Wazi |** Sura ya Maono Kibiblia na kitheolojia – kile Mungu anahitaji kanisa liwe na lifanye – vilitolewa kwenye kipindi cha 1. Hapa tunaeleza kazi ya kauli ya maono kwenye kanisa la mahali pamoja. Vidokezo vya ufunguo wa kauli ya maono ni kuwa vinaendana na yale ambayo Mungu anayafundisha katika Biblia, yanaelezwa kwa wazi yanaelezwa/ yanapelekwa kwa wengine tena na tena, na yanashilikiwa na wote, washiriki na viongozi.

**Kuchambua kauli ya Maono |** Waalike watu waainishe vile mfano wa kauli ya maono unavyoakisi funguo 8 za vidokezo/ishara. Je, zinatoa picha iliyo wazi ya tamanio la wakati ujao? Je, zinawawezesha watu kuyaona mambo kwa mtazamo/jicho la Ki-Mungu? Je, zinategemea makusudi ya Mungu ya ukombozi? nk.

## 1. MAONO YALIYO WAZI | 1Pet 2:9,12.

Kanisa huona kwa uwazi vile ambavyo Mungu anataka liwe na lifanye kama mwili wa Kristo, kwa vitendo katika mahali na muda maalumu. Maono haya yanaendana na makusudi ya Mungu ya ukombozi na huliongoza Kanisa kwenye dhamira yake. Katika Kanisa lenye afya, maamuzi kuhusiana na huduma, fedha, jengo nk yanafanywa juu ya msingi wa misheni/dhamira.

### Maelezo ya funguo 8 za hali ya maono.

1. Yanatoa picha dhahiri ya tamanio la wakati ujao
2. Yanawezesha mtu kufikiri/kuona uwezekano wa vitu kwa "miwani" ya Mungu.
3. Yana msingi juu ya makusudi ya Mungu ya ukombozi.
4. Hayaridhishwi na mambo yanavyoonekana kwa wakati uliopo.
5. Yanahitaji imani.
6. Yanaelezwa kwa namna iliyo rahisi
7. Yanamsogeza mtu katika maombi na vitendo/yanatoa hisia za ulazima.
8. Ni shirikishi (kati ya Viongozi na washirika)

### Kufafanua Kauli ya Maono:

*"Maono/Dira yetu ni kwamba kila mtu na kila familia katika mji wetu inapata fursa ya kumpokea Kristo kuwa mwokozi na Bwana, wanakua katika kumjua yeye na kutumia vipaji na rasilimali kwa utukufu wake"*

**Zoezi** | Pima Afya ya Kanisa Lako.

Soma kila maelezo na uonyeshe maoni yako. ("1" inaonyesha haukubaliani kabisa na maelezo; "10" inaonyesha unakubaliana kabisa na maelezo)

- Kanisa letu lina maono ya wazi na yanayoelezeka kwa wakati ujao unaotamaniwa.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

- Najisikia/nahisi kuvutiwa na maono ya Kanisa langu.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

## 2. KUIMARISHA UONGOZI | Efe 4:11-12

Kanisa linatumikiwa na Viongozi walioitwa na Mungu, wanaoelewa maono yao, wanayaeleza maono Kanisani kwa uwazi na kuwaandaa washirika kuyafanya maono yawe halisi (yatokee).

**Tabia za Viongozi katika maandiko:**

3. Kiongozi anatumwa na Mungu (Yn. 17:18)
4. Kiongozi ni mtumishi.(Fil 2:5-8; Mk 10:42-45, Yn 13:14-15)
5. Kiongozi hutafuta uongozi wa Mungu(Zaburi 25:4-5)
6. Kiongozi hutoa motisha na kuwaandaa watu wa Mungu (Efe 4:11-12, 2Tim 2:2)

**Tofauti za mitindo ya Uongozi:**

| KIONGOZI WA KIMABAVU | KIONGOZI MTUMISHI |
|---|---|
| Husema "Nifuateni" | Husema "Tumfuate Yesu" |
| Huamua maono na malengo yake kwa ajili ya Kanisa | Hutenda kazi pamoja na viongozi ili kupambanua maono na malengo aliyo nayo Mungu kwa ajili ya Kanisa. |
| Hagawi majukumu, hutoa amri tu | Huwahusisha wengine |
| Hufanya maamuzi peke yake | Huwakaribisha wengine ili kushiriki katika kufanya maamuzi |
| Hulalamikia madhaifu ya kusanyiko | Huliimarisha kusanyiko katika maeneo ambayo lina udhaifu. |
| Hufanya kila kitu yeye mwenyewe: kuhubiri, kutembelea, kuomba, kufundisha, kuongoza Ibada, nk. | Huwafunza wengine kufanya huduma na huwathibitisha |
| Anawaona viongozi wengine kama washindani na tishio kwake. | Anawaona viongozi wengine kama wabia na baraka kwake |

Kufikiri kwamba wachungaji ndio watu pekee wanaoweza kufanya mambo Kanisani, siyo tu ni upumbavu-bali si kibiblia. Katika Kutoka 18:13-27 Musa alipaswa kujifunza jinsi ya kuwaimarisha wengine kufanya huduma ili watu waweze kupata usikivu wanaouhitaji na yeye mwenyewe asije akachoka mno!.

**Tafakari**| Je, unawaweka wengine kufanya kazi? Ni nani unayeweza kumhusisha kwa njia tofauti  na Kanisa lako?

**Kuimarisha Uongozi |** Sisitiza kile Waefeso 4:10-12 inachokifundisha kuhusiana na kazi za viongozi kuwafunza na kuwahamasisha washirika wote kwa huduma. Kazi ya viongozi ni kujua maono ya kanisa, kuyaeleza kwa uwazi kanisani, na kuwaandaa washirika kutumia karama na raslimali zao ili kuyafikia maono hayo. Kipindi cha "fanya yote Mchungaji" kimekwisha unafika wakati wa mchungaji kuwa kama mwezeshaji. Mchungaji asijaribu tena kufanya kila kitu yeye mwenyewe, badala yake awaongoze watu wengine kuzitumia karama zao katika huduma. Kila mtu ana karama inayopaswa kutumiwa kuwabariki wengine ndani na nje ya kanisa.

**Zoezi** | Pima Afya ya Kanisa Lako.

- Kuna Viongozi wanaofunzwa na kuandaliwa kwa nafasi za uongozi kwa wakati ujao.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

- Viongozi wanawasaidia na kuwaongoza wale wenye shauku ya kuwa watendaji ndani ya Kanisa.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

**Mwili uliohamasishwa | Washirika wa kanisa hutenda kazi pamoja wakitumia karama zao sawasawa, ndani ya kanisa na katika jamii. Sisitiza umuhimu wa kila mtu kuchunguza karama yake ni ipi na aitumie.**

**Shirikisha simulizi ifuatayo| Wakati fulani kiongozi wa mafundisho ya Biblia alimpa kila mshiriki wa kikundi zawadi iliyofungwa. Akauliza, " Je, tufanye nini juu ya zawadi hizi? Kwa kweli, wote wakasema wazifungue. Ndani yake kila mtu akapata kipande cha …… fumbo (chemsha bongo).**

**Basi, kiongozi akawaelekeza nini cha kufanya ili kutumia vipande hivyo. Washiriki wakaelewa kwamba walitakiwa kuviweka pamoja vipande vya fumbo ili kuona ni kitu gani kitatokea. Wakavipanga vile vipande pamoja, lakini wakagundua kwamba kuna baadhi ya vipande havipo! Kiongozi wa mafundisho ya Biblia akawambia, " Sasa, tunapaswa kuwaleta watu wengi zaidi kwa Kristo, ili karama zao zitumike kukamilisha kazi ya Kanisa!"**

**Uliza |Kila Mkristo ana karama inayopaswa kutumiwa – je, unaijua karama yako? Je, kanisa lako linawasaidia watu kugundua karama zao na kuzitumia?**

**Kuwaongoza washirika katika huduma| Washirika wote wa kanisa lenu wanapaswa kulelewa katika uhusiano wao na Mungu (kufundishwa), kufunzwa kwa ajili ya huduma, na wasaidiwe kupata huduma ambayo kwayo watazitumia karama zao. Waongoze washiriki kufanya kazi na wenzao ama katika vikundi vidogo ili kuainisha njia ambazo kanisa lao linatimiliza kila aina ya huduma. Waombe kuainisha makundi ambayo yana shughuli za kutosha na yanayohitaji kuzingatiwa zaidi.**

## 3. MWILI ULIOHAMASISHWA (KANISA) | 1 KOR 12:7, 1PET 4:10– 11.

Washirika wa Kanisa wanafanya kazi pamoja wakitumia karama zao kwa kuwajibika kwa Kanisa na jamii. Mchungaji fanisi anajua kuwapa motisha na kuwahusisha washirika wa Kanisa. Anagawa majukumu kwa wengine ili nao waweze kuzitumia karama zao.

**Kazi yenye mafanikio kama timu inahusisha:**

1. Lengo lililo hai na wazi
2. Kazi iliyoundwa ili kufikia matokeo
3. Washirika wenye uwezo.
4. Kujitolea kwa washirika wote
5. Mazingira ya ushirikiano
6. Kiwango cha ubora
7. Uongozi wa  kitumishi.

**Zoezi** | Pima Afya ya Kanisa Lako.

- Kanisa linawasaidia washirika kugundua karama zao kwa huduma.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

- Nimefunzwa kutumika ama kuongoza ndani ya (Kanisa) na jamii.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

**Zoezi** | Kuwaendeleza Washirika Katika Huduma.

**MAELEKEZO|** Fikiria juu ya huduma zilizopo katika Kanisa lako na uorodheshe chini ya makundi yafuatayo.

| KUSANYA WATU | WAJENGE WATU | WAANDAE WATU | WAHAMASISHE WATU |
|---|---|---|---|
| Njia za kuwafanya watu waungane na Kanisa lako, kuwafanya wajisikie kukaribishwa na kuwaalika waingie katika uhusiano na Yesu Kristo (mifano: huduma maalum za Ibada, matamasha ya muziki, miradi ya huduma za jamii, kufanya urafiki na wasioamini, Uinjilisti wa nyumba kwa nyumba, nk). | Njia kuwafuata watu na kuwasaidia wakue katika imani yao (vikundi vya kujifunza Biblia, shuhuda ya jumapili, ushirika wa maombi, madarasa ya waongofu wapya, huduma za wanawake, mahusiano ya malezi/ushauri, nk). | Njia za kuwafunza watu huduma maalumu na kuwasaidia kuainisha na kukuza karama zao (warsha za Uinjilisti, madarasa yanayohusu karama za kiroho, semina za maombi juu ya fedha kwa familia, kuwafunza watu kuongoza sifa au kuhubiri, mafunzo kwa Viongozi wa vikundi vidogo, nk) | Njia ambazo watu wanazitumia karama zao ndani na nje ya Kanisa (kuandaa chakula, kutembelea familia, kuongoza nyimbo katika Ibada, kuongoza kanisa jinsi shughuli fulani ambayo wanaifanya vizuri/wana uzoefu nayo, kuwa na kambi ya mpira kwa ajili ya watoto wa ujirani; kufanya usafi wa Kanisa, nk). Kitu chochote ambacho watu wanaweza kukifanya kinaweza kuunganishwa ndani ya huduma za Kanisa. |

Sasa, pitia orodha yako ili kuona ni wapi ambapo Kanisa lako lina ufanisi zaidi na ni wapi unapaswa kuchukukua hatua.

| KUSANYA WATU | WAJENGE WATU | WAANDAE WATU | WAHAMASISHE WATU |
|---|---|---|---|
| | | | |

**Ukiwa pamoja na Viongozi wa Kanisa lako, rudieni zoezi la kuwaendeleza washirika katika huduma:**

1. Orodhesha shughuli ambazo Kanisa lako linazo kwa kila aina ya huduma.
2. Jiulizeni kama shughuli mlizoorodhesha kwa kila kundi zina ufanisi katika eneo hilo.
3. Amueni ni wapi mnahitaji kuchukua hatua na nini kinapaswa kufanyika.

**4. UWAKILI WA RASILIMALI** | 1 Kor 4:2, Mith 3:9 – 10, 1 Kor 6:16-20, Mdo 20:35b.

Kanisa linawapa changamoto washirika wake kuwa mawakili wema wa mali na bidhaa zake na za kwao vile vile. Wakristo wote wanaweza kutumia rasilimali hizi (muda, vipaji, na hazina) kuendeleza kazi zao katika Ufalme wa Mungu, ndani ya Kanisa na katika jamii.Kanisa lenyewe linapaswa kutumia rasilimali zake kwa hekima na kwa unyoofu/uwazi.

**Mambo manne yanayohusu uwakili:**

1. **MUDA**
2. Kipaji
3. **HAZINA**
4. Hekalu la Mungu (miili yetu)

**Zoezi** | Pima Afya ya Kanisa Lako.

- Kanisa letu lina uwakili mzuri kwa namna linavyosimamia bajeti yake vyema.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

- Kanisa letu linafundisha mara kwa mara juu ya uwakili wa zaka.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

**Uwakili wa Raslimali |** Kanisa linawapa changamoto washirika wake kuwa mawakili wazuri wa raslimali zao muda, hazina, vipaji na hekalu la Mungu (miili yetu) ili kupanua ufalme wa Mungu ndani ya kanisa na katika jamii. Kanisa lenyewe vile vile linapaswa kuwa wakili mwema wa raslimali zake.

**Mifano ya Uwakili |**
- Kanisa linatunza vizuri jengo lake na mali zake.
- Mashemasi au kamati maalumu wahesabu na kusimamia fedha sio Mchungaji. Wanatunza kumbukumbu sahihi ya zaka na dhabihu na kutoa ripoti kwa kanisa jinsi fedha ilivyotumika.
- Kanisa linawatia moyo kutumia muda wao vyema (kuangalia familia, kazi, kutumika kanisani na katika jamii).
- Kanisa linaanda bajeti inayoendana na maono yake.

Kanisa lenye nguvu mara nyingi lina mipaka katika raslimali zake na linawekeza vile lilivyo navyo katika huduma na misheni yake. Sio kujilimbikizia raslimali kwa ajili yake lenyewe.

Waombe washiriki kutoa mifano ya namna kanisa lao linavyowasaidia watu kuutumia muda wao, vipaji vyao, hazina na hekalu lao (mwili) ipasavyo.

Waombe kuwashirikisha wenzao namna makanisa yao yanavyosimamia bajeti na utunzaji wa mahesabu.

### 5. **MUUNGANIKO KATI YA ANDIKO NA MUKTADHA** | 2 Tim 3:16-17; Mdo 17:22-23; 1 Kor 9:19-22; Mt 9:35-38.

Kanisa lenye afya linajali muktadha wake (eneo la kijiografia, jamii na njia ya kiuchumi, utamaduni, nk). Wakati ujumbe wa habari njema za Yesu Kristo haubadiliki, mbinu za kuushirikisha /kuueneza zinabadilika.

**Zoezi** | Pima Afya ya Kanisa Lako.

- Kanisa letu linaelewa mahitaji katika muktadha wa jamii yetu

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

- Kanisa letu linahitaji kujenga mahusiano na jamii.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

**Hitimisho:**

Kila Kanisa lina haiba yake na uwezo wake wa kipekee. Kanisa lililo imara katika maeneo matano tuliyoyajadili katika kipindi hiki litaongozwa na Roho Mtakatifu kuleta tofauti katika jamii yake kwa jina la Yesu litawaleta watu ili wapate maisha mapya katika Kristo na kuwasaidia kuishi ndani yake, kwa kumpa Mungu utukufu.

Sisitiza muktadha tofauti wa kijamii, kiuchumi na kiutamaduni unaopaitkana katika nchi tofauti, majimbo, majiji, miji na ujirani. Eleza ni jinsi gani tofauti hizi zinaathiri uinjilisti wa kanisa, ibada ,shirika, maono, kazi nk.

**IITim. 3:16-17** | Neno la Mungu ni mwongozo wa maisha.

**Mdo 17:22-23** | Paulo anaandaa ujumbe wake ili ufae kwa watu na mahali husika.

**1Kor. 9:19-22** | Paulo anajihusisha na watu kwa njia wanayoielewa ili awafikie kwa injili.

**Shughuli ya Hiari** | Washiriki wafikirie kati ya maeneo matano ni eneo lipi ambalo kanisa lao lina nguvu zaidi na eneo lipi kanisa lao ni dhaifu zaidi. Waruhusu washirikishane kila mmoja na mwingine katika makundi ya watu 3 au 4. Waombe wachague eneo moja la kushughulikia na wachangie mawazo jinsi kanisa linavyoweza kujikwamua katika eneo hilo.

## MAONI/KUMBUKUMBU |

KIPINDI CHA 3

# KAZI TANO ZA KANISA LENYE AFYA

**UTANGULIZI:**

Kipindi cha 3 kinatoa maelezo ya kazi tano za Kanisa lenye afya: Ibada, Uinjilisti, Uanafunzi, na Ushirika. Kutathimini Kanisa kwa maelezo ya kazi hizi huwasaidia Viongozi katika kupanga kwao kimkakati.

**Kazi Tano Muhimu** | Mdo 2:42-47




Kila kazi ina athari juu ya nyingine.

## 1. UINJILISTI | MDO 2:47; 2TIM 4:1-2, MDO 5:42, KOR 1:28-29.

Kanisa linatangaza kwa maneno na matendo ili watu waweze kuelewa kwamba Ufalme wa Mungu umekuja kupitia kwa Yesu Kristo. Linawaita kuamini habari njema, kuyageuza maisha yao kwa Yesu na kuwa wafuasi wake. Maisha yetu yanatoa ushahidi wa kiumbe kipya ndani ya Kristo – "Tangazo lililo hai" la yale ambayo Mungu amefanya.

NI Mungu anayelikuza Kanisa. Roho Mtakatifu hutenda kazi katika mioyo ya watu akiwaongoza kupokea uzima unaotolewa katika Kristo.

**Maswali ya kurejea:**

- Je, umewahubiiria Injili watu wangapi miezi miwili iliyopita?
- Je, Kanisa letu limewafunza waamini wangapi jinsi ya kushirikisha imani yao?

**Aina tatu za mabadiliko yanayohitajika kwa watu wafikie kumjua Kristo:**

1. MABADILIKO YA NGUVU | Watu wanatambua udhaifu wao binafsi na kupokea nguvu za Mungu katika maisha yao kupitia kazi ya Roho Mtakatifu, akiwapa uzima, akivunja nguvu ya dhambi katika maisha yao, na kuwaletea tunda la Roho: upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, utu wema, uaminifu, upole na kiasi.
2. MABADILIKO YA IMANI | Maisha yetu yanafunguliwa ili kukubali kwamba Yesu ndivyo alivyo kama Biblia inavyosema: Mwana wa Mungu aliyefufuka. Watu wanafikia kugundua kwamba Mungu hunena kupitia maandiko na kuwa yale anayosema yanaweza kuaminiwa.
3. MABADILIKO YA UTASHI | Watu wanayaelekeza maisha yao kwa Kristo na kujinyenyekesha kwenye mapenzi yake katika maeneo yote ya maisha yao.

**Zoezi** | Pima Afya ya Kanisa Lako.

Soma kila maelezo na uoneshe maoni yako. ("1" inaonesha haukubaliani kabisa na maelezo; "10" inaonesha unakubali kabisa)

- Kanisa letu linawafunza na kuwaandaa washirika wake kutoa ushuhuda kwa jamii.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

- Najisikia kuhusika kibinafsi na kazi ya kiinjilisti ya kanisa letu

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

**Ufuatiliaji pamoja na viongozi wa kanisa lako.**

- Je, kanisa lako linawatiaje moyo watu kuziona nguvu za Mungu, kusikia ukweli wa Mungu na kuitikia kwa moyo wote wa kujitolea kwa Kristo?

## 2. UANAFUNZI | MDO 2:42; MT 28:18-20; 2PET 3:18

Kanisa lenye afya linawasaidia watu wa rika zote kumjua Kristo na mapenzi yake vyema ili waweze kumfuata katika maeneo yote na hali zote za maisha yao ya kila siku. Kadiri tunamvyojua yeye na mapenzi yake na kumtegemea Roho wake tunaendelea kufanana na Kristo zaidi na zaidi katika:

1. Mwenendo wetu
2. **KUFIKIRI** kwetu
3. Tabia zetu
4. **KUJITOA** kwetu.

**Mchoro** | Imani iliyogawanyika dhidi ya Imani Iliyounganishwa




Imani iliyogawanyika | Imani iliyounganishwa

**Zoezi** | Pima Afya ya Kanisa Lako.

- Wakati mwongofu mpya anapompokea Kristo, papo hapo anapata mtu wa kumfuatilia/kumlea.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

- Kanisa linanisaidia kukua kiroho.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

**Ufuatiliaji pamoja na Viongozi wa Kanisa lako:**

- Je, Kanisa letu linawasaidiaje watu kukua katika uhusiano wao na Yesu Kristo?

- Je, Kanisa letu linatoa fursa zipi kwa watu kujifunza maandiko na

**Uanafunzi** |
• Mwenendo (mwenendo wetu ufanane zaidi na zaidi na wa Yesu: Fil. 1:17, Ef. 5:1-2)
• Kufikiri (tunaakisi tunda la Roho: Gal. 5:22-24, Efe. 5:1-2).
• Kujitoa (tunajitoa nafsi zetu kwenye mapenzi ya Mungu pasipo kujali gharama: Mt. 26:29, Yn. 6:38).

**Imani iliyogawanyika** | Imani ni sehemu nyingine tu ya maisha yetu. Tunawaza ya Mungu tunapomwabudu tu, lakini siku nyingine zilizobaki tunaendelea na maisha yetu pasipo kumtafakari. Hatuwazi jinsi Mungu anavyohusika na uhai wa familia zetu, fedha zetu, siasa, michezo nk.

**Imani iliyounganishwa** | Imani yetu katika Yesu ina matokeo/ inaathiri namna tunavyozitendea familia zetu jinsi tunavyoishi katika jamii zetu na taifa letu, namna tuavyoshiriki michezo, tunavyosimamia fedha zetu nk. Kwa kila eneo la maisha, tunatafuta kumpendeza Mungu.

kuyatumia katika maisha yao?

- Wanisa letu lina fursa zipi kwa ajili ya watu kuomba pamoja na kuombeana wao kwa wao?

- Je, kanisa letu linawasaidiaje washiriki kujifunza kumfuata Yesu katika maisha yao, kufanya maamuzi yao, kazi zao za kila siku, matumizi yao ya fedha, na matumizi yao ya muda?

### 3. **HUDUMA** | Mdo 2:45-46, Gal 6: 10, Mk 12:31, Yak 2:17

Kanisa linakutana na mahitaji ya watu na jamii kwa ukamilifu wake kupitia Kristo na kuwaalika ili wawe wanafunzi wake.

KItabu cha Yakobo kinaweka wazi kwamba imani pasipo matendo imekufa (Yakobo 2:17). Tunawatumikia wengine sio kwa ajili ya kupata/kugharimia wokovu, bali kutokana na shukrani kwa yale ambayo Mungu ametutendea. Kuwatumikia wengine kwa zawadi na rasilimali zetu ni ushahidi ulio dhahiri wa upendo wa Mungu kwao. Serving others with our gifts and resources is the visible proof of God's love for them.

**Muunganiko| Uhusiano kati ya huduma na Uinjilisti:**

1. Huduma ni matokeo ya Uinjilisti: upendo wa Mungu hutufanya tutamani kuwatumikia wengine.

2. Huduma ni daraja la kutufikisha kwenye Uinjilisti: Tunatia zege ya huduma kwanza, na yale matendo ya huduma yanafungua mlango wa kushirikisha imani yetu.

3. Huduma kufuatana na Uinjilisti: Tunapowatumikia wengine, tunanena habari za upendo wa Mungu kwa ajili yao katika Kristo.

**Zoezi** | Pima Afya ya Kanisa Lako.

- Kanisa letu linawasaidia watu kwa mahitaji yao ya kimwili.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

- Watu wa jamii wanajua kuwa tunataka kudhihirisha upendo wa Kristo kwa njia za matendo.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

**Ufuatiliaji pamoja na Viongozii wa kanisa lako:**

- Je, washirika wa kanisa letu wanaitumikiaje jamii yake?
- Je, kanisa letu kwa ujumla linaitumikiaje jamii yetu?

**4. USHIRIKA** | Mdo 2;42, 44, 46, Gal 6:2, Efe 4:25-26 na 5:2

Kwenye kanisa lenye afya, wanafaidiana na kubebeana mizigo, wanaonyeshana upendo na huruma ya Mungu. Hii ina maana tunatakiwa kufahamiana na kushirikishana katika maisha ili tuweze kujua njia bora za kusaidiana. Neno la kiyunani kwa neno la ushirika, koinonia humaanisha "kwa wote". Ushirika wa mkristo ni wa kwanza kuwa na Kristo kwa wote, na kwa sababu ya hilo, tunashirikisha vile tulivyo na vile tulivyo navyo kwa ndugu zetu na dada zetu katika Kristo. Vikundi vidogo ni njia moja ambayo wakristo wanaweza kusaidiana na kukua pamoja katika imani yao.

Makanisa yenye afya yanaelewa kuwa migogoro ni sehemu ya kawaida kama kanisa. Wanasuluhisha migogoro kwa njia ya kujenga, wanalenga jinsi ya kushughulikia hali hiyo ili kanisa liendelee na uaminifu kwaa maono yake na huinena kweli katika upendo. Viongozi wanapaswa kuwa wenye upendo na wastahivu lakini walio imara. Pale washirika ama viongozi wanapoenenda pasipo kufuata mwongozo wa kibiblia, wanahitaji kusahihisha kwa umakini, lakini kwa msimamo.

a. **YOHANA 17 |** Misingi ya kitheolojia ya ushirika inatokea kwenye utatu wenyewe – jamii ya kwanza.

b. **ZABURI 133 |** Tangu Agano la Kale (AK) tunaona manufaa yanayotokana na umoja kati ya waaminio.

**Zoezi**| Pima Afya ya Kanisa Lako.

- Huduma za Kanisa huwasaidia washirika kukua katika uhusiano wa kirafiki na wengine.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

- Kuna ushirika mzuri katika Kanisa letu.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

Katika ulimwengu uliojaa ukiwa, upweke, utengano na vurugu, ni sharti kanisa liandae jamii yenye upendo, upatanisho, neema na msamaha.

Waombe washiriki kutaja njia nyingine ambazo washirika wanaweza kufahamiana na kusaidiana wao kwa wao.

**Jinsi viongozi wanavyoweza kushughulikia migogoro ndani ya Kanisa |**

1. Pambanua mgogoro (watu wanatofautiana nini).
2. Chambua mgogoro kadri uwezavyo pasipo upendeleo: Vyanzo vyake, tabia zilizoongoza mgogoro, nk. Usiruhusu watu kushambuliana wao kwa wao kwa maneno – lenga tabia, sio watu.
3. Ainisha mambo yanayofanana kwa pande zote mbili zinazopingana
4. Ainisha njia zitakazosuluhisha mgogoro.
5. Chagua njia inayoaminika zaidi kwenye amri za Mungu katika maandiko, kwenye maono ya misheni ya kanisa na inayofaa zaidi kulingana na hali.
6. Waalike watu kuomba msamaha na kutoa msamaha/ kusamehe.
7. Tekeleza uamuzi.

**Ufuatiliaji pamoja na Viongozi wa Kanisa lako:**

- Je, ni kwa kiwango gani ndugu katika Kristo wanafahamiana ndani ya Kanisa?
- Je, tumewaonaje wakisaidiana na kutiana moyo?
- Je, Kanisa letu lina mpango wa kushughulika na migogoro?
- Ni mgogoro gani mkubwa wa mwisho kutokea Kanisani kwetu na ulisuluhishwa vipi?

**5. IBADA** | Mdo 2:42a, Zab 47:1; Zab 48:9, Rum 12:1-2.

Kanisa hukusanyika pamoja kama familia ya Mungu ili kumsikiliza Mungu na kumwitikia Mungu kupitia sifa, ungamo, shukrani, na maombezi. Katika Ibada tunaukiri ukuu wa Mungu na kujitolea sisi wenyewe kwake.

Huduma ya Ibada ni muda maalum ambapo watu wa Mungu wanakusanyika ili kukutana na Mungu kwa pamoja. Jambo hili ni la kipekee ambalo kwalo Mungu anasema na watu wake na watu wake kusema na Mungu:

- Mungu anatuita kumwabudu yeye – tunaitikia kwa kumsifu kwa pamoja.
- Mungu anatuita kuungama dhambi zetu-tunaitikia kwa kuungama dhambi zetu na kuomba msamaha/toba – Mungu anasamehe kupitia kwa Yesu Kristo.
- Mungu hunena nasi kupitia neno lake – tunaitikia kwa ukiri wa imani, dhabihu, shuhuda, na maombi.
- Mungu huonesha upendo wake katika Sakramenti (Ubatizo na Meza ya Bwana) – tunapokea kazi ya Mungu kupitia kwa Roho wake Mtakatifu.
- Mungu hutubariki na kututuma katika Ulimwengu – tunatoka katika eneo la Ibada ili kumtumikia Mungu katika shughuli zetu za maisha. Vifungu vya mwanzoni vya Rumi 12 vinaonyesha kwa upana kuwa Ibada inahusisha maeneo yote ya maisha. Tunaishi siku zote katika uwepo wa Mungu, tukiitikia wema na ukuu wake.

**Sababu za Ibada zinazoweza kusaidia Kanisa kukua:**

1. Ukaribisho mzuri kwa wageni (kuhakikisha wanapata mahali pa kukaa/kusimama na maelekezo ili wajue ni nini kinachoendelea)

2. FUfuatiliaji wa wageni (simu/kuwasiliana nao binafsi mara tu

wanapohudhuria Ibada).

3. Nafasi kwa ajili ya watu katika eneo la Ibada.

4. Mahubiri ya Kibiblia yenye nguvu yanayoendana na maandiko na yenye uhusiano na maisha ya watu.

5. Mawasiliano yaliyo wazi juu ya njia ambazo watu wanaweza kujihusisha ndani ya Kanisa.

**Zoezi** | Pima Afya ya Kanisa Lako.

- Ibada katika Kanisa letu zinatukuza na kutuimarisha katika maisha yetu ya Kikristo.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

- Katika huduma zetu za Ibada utatu wa Mungu unatambuliwa: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|

**Ufuatiliaji pamoja na Viongozi wa Kanisa lako.**

- Je, Ibada zetu ni zenye heshima na furaha?

- Je, tunazitumia kwa utukufu wa Mungu?.

- Je, tunaweka msisitizo zaidi juu ya kipengele kimoja (Muziki, Viongozi maalum, nk).

**Uchambuzi | Kazi Tano**
Baada ya washiriki kujaza chati wape nafasi waainishe eneo ambalo kanisa lao lina nguvu kati ya zile kazi tano na eneo ambalo kanisa lao ni dhaifu kabisa. Waruhusu washirikishane na wenzao katika vikundi vya watu 3 au 4. Muda ukiruhusu, washiriki watoe maoni ya namna ya kuboresha maeneo yaliyo dhaifu zaidi..

Kuna vipengele vingine muhimu katika ukuaji wa kanisa ambavyo viongozi watavitumia katika kufanya maamuzi yao, kama vile muundo, mipango na mawasiliano, na muktadha wa kiroho ambao kanisa limo. Tutashughulika na baadhi ya hivi katika kipindi cha 4.

**Uchambuzi** | Kazi tano.

Kwa kila kazi onesha huduma za Kanisa lako:

| UINJILISTI | UANAFUNZI | HUDUMA | USHIRIKA | IBADA |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

1. Ulipomaliza kujaza chati, Je, umegundua maeneo uliyo na nguvu na uliyo na udhaifu?

2. Je, chati inaonesha mtazamo wenye uwiano mzuri katika huduma?

# KIPINDI CHA 4.
# MFUMO WA MABADILIKO

Mfano wa msitu na miti unarejea ukweli kwamba ili kutumika vyema, viongozi wa kanisa wanahitaji kueleza sio tu kila sehemu ya huduma (miti), bali pia huduma kwa ujumla wake (msitu).

## UTANGULIZI

Kutokana na jamii za kitabibu na kisayansi tumejifunza kuhusu viumbehai kama mifumo – mfumo mzima wenye sehemu zinazoingiliana kiutendaji ndani ya kiumbe hai na nje ya kiumbe hai. Ufahamu huu na jinsi mifumo inavyofanya kazi unaweza kupatana/kutumiwa na mashirika.

Kanisa ni kiumbe hai – mwili ni Mkristo – na ni shirika. Lina sehemu nyingi na ni mwili wa tofauti wenye mifumo mingi midogo, na inaingiliana katika mazingira fulani fulani. Kuna hali ya kutegemeana na kuhusiana kati kati ya mifumo yote midogo midogo inayounda mfumo mmoja mkubwa. Mfumo huu mkubwa hutenda na kuathiri mifumo mingine na mazingira yake.
Unapoona picha hii kubwa ya mahusiano yenyewe kwa yenyewe na mwingiliano na mazingira ni mtazamo unaoitwa "mifumo iliyo wazi". Dhana hii inatusaidia kuwa na njia za vitendo na zenye afya ili kuanzisha na kuendeleza kazi ya "kuwafanya wanafunzi"na kufanya mabadiliko ya lazima kama Kanisa linalolenga dhamira.





Unapaswa kuuona mti na vile vile msitu

**KANUNI |** Kanisa ni kiumbe hai kama mwili wa Kristo, na kwa wakati huo huo lipo kama shirika lililo hai, linaloonekana (makusanyiko, Madhehebu) ambapo kwayo Mungu anatenda kazi katika ulimwengu. Kadri tunavyoendelea kufahamu namna shirika linavyofanya kazi, ndivyo tutakavyolisaidia kusanyiko letu kutenda kazi vizuri zaidi.

**Zoezi** | Namba zilizochanganywa.

Una sekunde 30 za kutafuta namba na kuzizungushia/kuziwekea duara (kuanzia namba 1) ili kuona utafikia umbali gani. Itafute namba 1, izungushie duara, kisha 2, izungushie duara, na kuendelea.

Andika hapa namba ya juu uliyoizungushia: ____________________



## Hii inatuonesha umuhimu wa:

- Mipangilio
- Utaratibu
- Ufanisi
- Ubunifu
- Kuelewa mfumo/mpango wa shirika.

**Zoezi la Namba zilizochanganywa** | Fuata maelekezo yaliyotolewa kwenye kitabu cha washiriki. Wape watu sekunde 30 kutafuta namba na kuzizungushia duara kwa mpangilio, kuanzia 1, na uone wanaweza kufikia umbali gani. Wataitafuta # 1, waizungushie duara, kisha # 2 na kuiweka duara, # 3, waizungushie duara na kuendelea mpaka muda utakapokwisha. Mwishoni mwa sekunde 30, waombe watu waandikie namba ya juu kabisa walioifikia.

Kisha fanya sehemu ya pili ya zoezi. Wakati huu, waombe wafanye kitu kile kile (kuzungushia namba ili kuona wanafikia umbali kiasi gani) lakini waeleze vidokezo viwili vifuatavyo kabla hawajaanza kuzungushia duara:

a. Namba zimegawanyika katika robo duara nne. Namba 1-6 zinapatikana kwenye nusu ya juu, sita zinazofuata (7-12) zinapatikana kwenye nusu ya chini. Namba sita zinazofuata (13-18) zinapatikana kwenye nusu ya juu, kisha sita zinazofuata (19-23) zinapatikana kwenye nusu ya chini na kuendelea.
b. Vile vile hakuna namba mbili zinazofuatana zitakazopatikana kwenye kisanduku kimoja. Hivyo, kwa mfano, namba 1-6, zilizo kwenye kisanduku kimoja. Hivyo kwa mfano namba 1-6 , zilizo kwenye nusu ya juu zinabadilika kulia na kushoto.

Baada ya kuwaeleza watu kanuni hizi mbili, rudia zoezi, wape watu sekunde 30 kuwekea duara namba nyingi wawezavyo. Baada ya sekunde 30, waombe watu wainue mikono ikiwa wamefikia idadi kubwa ya namba awamu ya pili .Karibu kila mtu atafikia idadi ya juu. Waulize washiriki kwa nini wamefikia idadi ya juu zaidi awamu ya pili. Wanaweza kusema awamu ya pili walielewa mfumo, au walijua jinsi namba zilizopangwa, nk.
Kusudi la zoezi hili ni kuonesha thamani ya kufahamu jinsi mfumo ulivyopangiliwa. Kwa njia iyo hiyo, kuelewa viwango vya jinsi kanisa linavyokua kunaweza kutusaidia kuwa na ufanisi zaidi katika huduma aliyotupa Mungu.

## SEHEMU ZA SHIRIKA.

**Mchoro 1** | Hali za nje zinazoathiri kusanyiko/Kanisa




- Baadhi ya hali za nje zinabadilishika na zinanyumbulika.
- Baadhi ya hali za nje hazibadiliki – ziko pale pale.

### Shughuli:

Toa mfano wa hali za nje zilizo na athari kwa kusanyiko lako. Je, zinabadilishika au ziko pale pale/za kudumu?

### Ufuatiliaji pamoja na Viongozi wa Kanisa lako:

- Bainisha hali za Kanisa zenye athari na zinazoliumba Kanisa lako. Zipi zinabadilika zaidi? Zipi zisizo na mnyumbuliko?

**Sehemu za Shirika | Vigezo/Mipaka**

Hii ni mipaka ya nje ya kiumbe hai inayolitofautisha na viumbe vingine. Maadili ya Kibiblia, mapokeo yetu fulani ya kidini na historia ya shirika letu na maadili yanatutambulisha sisi ni nani na nini tutakachokifanya.

Kwa mfano, kanisa lenye afya litafuata mipaka ya Kibiblia na halitaruhusu washirika wake kusengenyana (Law. 19:16, Zab. 34:13, Yak.4:!1). Mipaka pia inahusisha mipaka ya kuonekana kama vile ya jengo la kanisa na raslimali.

- Baadhi ya vigezo|hali zinabadilika na kunyumbulika. Matendo ya kiutamaduni na tabia za kusanyiko zinaweza kubadilika. Mapokeo ya dini yanabadilika kwa njia mbalimbali na maadili yanaweza kubadilika tunapoendelea kukua zaidi kulingana na vile Mungu anavyotuita tuwe.
- Baadhi ya hali hazibadiliki ziko vile vile. Kwa mfano, maagizo ya Kibiblia hayabadiliki"

**Muktadha |** Kila kiumbe hai kinaishi katika hali fulani. Kila kusanyiko hujikuta mahali fulani, kwa wakati fulani. Kuwa makini na mazingira yetu (utamaduni wetu, mtindo wa maisha ya watu, nk) hutuwezesha kupeleka Injili kwa ufanisi zaidi.

**Shughuli za Ufuatiliaji |** Ruhusu viongozi wa kanisa lako waorodheshe kila kitu wanachokifahamu juu ya watu katika ujirani wako (mivuto yao, mahitaji nk). Wasaili majirani ili kuwafahamu zaidi na mtazamo wao ulivyo juu ya kanisa.

**Kumbuka |** Hii ni sehemu ya kiufundi zaidi katika warsha nzima.kama unapata shida kuelewa michoro ama unadhani hazitafaa kwa wasikilizaji, jisikie huru kwenda moja kwa moja kwenye zoezi la "Zulia Jekundu" katika ukurasa wa 28 wa Kitabu cha Mshiriki.

**Dhana za mfumo |** Shirika lina vidokezo/sehemu za ndani na za nje. Wakumbushe washiriki kuwa kanisa la kitaasisi ni shirika linaloonekana linalotafuta kuwabadilisha watu na jamii kwa utukufu wa Mungu na ukuaji wa kanisa la Yesu Kristo.

Chini kuna maelekezo ya sehemu za shirika na dhana za ufunguo za mfumo ambazo zimeorodheshwa kwenye kitabu cha mshiriki. Eleza sehemu na dhana hizi kwa kuunganisha na michoro ya ukurasa wa 25 -27 wa kitabu cha mshiriki. Tumia mifano yako binafsi ili kusaidia kuelezea sehemu na dhana.

**Sehemu za Ndani |** Makanisa kama mashirika, yana sehemu nyingi zinazoathiri utendaji kazi. Viongozi, mipango, washirika, na raslimali zote zina matokeo, yawe chanya ama hasi. Kanisa lipo chini ya uongozi wa Kristo, na kusudi lake ni kutangaza na kuiishi injili kwa namna ambayo watu wengine watafikia kumjua Kristo kuwa ni Bwana. Ndani ya kanisa kuna mifumo mbalimbali midogo midogo kama vile uongozi, mfumo wa ki-shirika, washirika, mipango, njia za mawasiliano na matumizi ya raslimali. Mifumo hii midogo midogo inapoelekezwa katika misheni ya kanisa na ikafanya kazi vyema, maisha ya watu na jamii zitabadilika kwa nguvu ya Injili.

Jambo fulani linapokwenda vibaya katika mfumo mdogo mmoja, mifumo mingine huathirika pia. Hii ni kwa sababu mifumo midogo midogo inahusiana na kutegemeana.

## Mchoro 2 | Hali za ndani za kusanyiko/Kanisa

**KANISA| AMBALO KRISTO NI KICHWA**
KIUMBE HAI |SHIRIKA.




**MTIRIRIKO WA WATU |** UKARIBISHO– KUJIHUSISHA – HUDUMA.

- Katika kila Kanisa kuna mifumo midogo midogo inayoathiri namna Kanisa linavyotenda kazi

## Shughuli:

Bainisha baadhi ya mifumo midogo midogo ya kusanyiko lako (mipango, huduma, kamati,nk). Je, zinahusianaje?

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

## Ufuatiliaji pamoja na Viongozi wa Kanisa lako:

- Bainisha sehemu tofauti za Kanisa lako, baraka na changamoto za kila sehemu.

**Muunganiko na |** Sehemu za mfumo zinahusiana na zinaathiriana. Katika kusanyiko, kitu kinachotokea katika eneo moja la maisha ya kanisa, kinaathari juu ya sehemu nyingine. Kwa mfano, tatizo linalohusiana na fedha, linaweza kuleta changamoto kwa mipango mingine, wakati waumini wengi zaidi wanapozitumia karama zao waweza kuwa Baraka katika mipango ya kanisa.

**Kusudi |** Kila mfumo una kusudi fulani. Kusudi la kaniska linapimwa kwa kile ambacho Mungu anafundisha katika maandiko: kutangaza habari njema za uzima katika Kristo na kuwafundisha watu kuishi sawa sawa na mapenzi ya Mungu (Mt. 28:19-20). Kanisa linapopuuza misheni hii ya kufanya wanafunzi linakosa kuishi sawasawa na mpango wa Mungu.

**Uthabiti |** na uwezo wa kubadilika | Kila mifumo ina hali ya kutokukubali mabadiliko. Ndani ya kanisa mara nyingi tunasikia watu wakipinga mawazo mapya kwa sababu "hatujawahi kufanya namna hiyo". Watu wanapenda kufanya mambo kwa njia walizozizoea kuliko kujifunza njia mpya. Viongozi wanatakiwa kutafuta njia za kuwasaidia, washirika kuelewa mabadiliko na kuyajadili na kuhakikisha kiwango cha mabadiliko kinafaa.

**Unyambulifu |** Zinaweza kuwepo njia nyingi za kufikia lengo. Hii inasaidia mifumo kunyumbulika na kufanya marekebisho. Kwa mfano: inawezekana kanisa haliwezi kununua vyakula kwa ajili ya wamama wasio na waume katika ujirani, lakini linaweza kuwa na baadhi ya watu wanaoweza kusaidia shughuli za watoto wanapotoka shule wakati wamama hawa wakiwa kazini.

**Mipango Mbadala |** Mashirika yanatenda kazi katika mazingira yasiyotabirika na hivyo yanahitaji kuweka mipango mbadala-mipango ya kufanyia kazi ikiwa mpango wa kwanza haukufanikiwa. Mfumo wenye afya una mipango mbadala ili uendelee kufikia malengo wakati mambo yanapokwenda vibaya. Kwa mfano, kanisa linapanga kufanya uinjilisti wa nje, itakuwa jambo la hekima kuweka "Mpango B" ikitokea mvua ikanyesha.

**Mchoro wa 3** | Hali za Nje na Ndani – Mabadilko




- Mabadiliko chanya katika Kanisa na jamii yanaonekana kama sehemu za ndani za kusanyiko zinazoitumikia dhamira/Misheni ya Kanisa kwa namna inayofaa kulingana na muktadha (mazingiria).

- Mabadiliko chanya yanapunguza mwendo ama kisimamishwa pale sehemu za ndani za kundi zinapokosa kuongozwa/kuelekezwa kwenye ono lake na Misheni yake.

## DHANA MUHIMU ZA MIFUMO

- Muktadha
- Muunganiko na kutegemeana
- Kusudi
- Uthabiti na uwezo wa kujirekebisha sawa sawa na mazingira (unyambulifu)[1]
- Njia ya kufanikisha/kuyafikia matokeo yale yale kwa kutumia njia mbalimbali[2]
- Mipango mbadala ikiwa mpango wa awali haukufaulu[3]
- Muundo na vigezo.

Kanisa lenye afya litakuwa na njia za kuwakaribisha wageni/wongofu wapya kuwahusisha, kuwalea katika imani yao, na kuwasaidia waanze kuzitumia karama zao.

Kanisa lenye afya na linalokua litahakiki mara kwa mara sehemu tofauti za mfumo wake. Litajifunza zaidi kuhusiana na muktadha wake, litatathmini jinsi mipango yake inavyoendelea, litachunguza ili kuhakikisha raslimali zinatumika vizuri nk.

1 Uwezo wa kiumbe hai kujirekebisha mazingira yake ya ndani ili kuendeleza hali fulani.
2 Uwezo wa matokeo yaleyale kupitia namna/mbinu tofauti/mbalimbali.
3 Mipango ya kutekeleza ikiwa mpango wa kwanza haukufaulu.

**Mabadiliko |** Kila mfumo unatumika kwa kusudi fulani. Kusudi la kanisa ni kuwaongoza watu kukutana na Yesu, ili ayabadilishe maisha yao na jamii.

Mchoro huu unaonesha hali |Sehemu za nje na ndani katika picha moja.
- Nini kitatokea kama familia mpya 5, 10 au 20 zitajiunga na kanisa lako.
- Kati ya watu wapya/wageni wanaokuja kanisani, je, panaweza kuwepo na baadhi wenye karama za uimbaji au kuongoza ibada?
- Je, wale watakaojiunga watakuwa watu wazuri, wenye kukubalika?
- Je, watakuwepo wachache wenye maoni yenye nguvu?
- Je, watakuwepo wachache wenye matatizo mazito?
- Je, watakuwepo baadhi wenye kusengenya?

Maswali haya yawasaidiie washiriki kufikiria jinsi ambavyo ukuaji ungeathiri kanisa lililopo. Kanisa lenye watu 80 ambalo linaongezeka watu wapya 20 au 30 kwa mwaka litakutana na mabadiliko ya kiwango cha juu na matokeo katika mfumo wake. Ni muhimu kwamba uongozi wa kanisa uwe umejiandaa kushughulika na matokeo haya kwa njia ya afya inayoruhusu kanisa kukua. Vinginevyo watu watapungua na kanisa halitakua. Kuna mifano miwili unayoweza kuitumia kusisitiza umuhimu wa uwiano katika ukuaji wa kanisa.

- Ukiongeza chumvi zaidi kwenye supu, inabadilika ladha. Unaweza kuongeza chumvi zaidi, lakini kwa sehemu utapaswa kuongeza maji zaidi, mboga za majani, nyama na michanganyiko mingine ili kutunza uwiano wa ladha. Huwezi kuendelea kuongeza chumvi tu.
- Mwili wa mwanadamu ni mfumo unaohitaji uwiano ili kuendelea na afya yake. Ikiwa moyo wako uko katika hali njema, lakini ini lako haliko vizuri/salama, halitasaidia moyo kuwa thabiti. Unahitaji ogani zote ziwe na afya ili uwe salama.

**Zoezi | Zulia jekundu**

Zoezi hili ni sehemu ya muhimu zaidi katika kipindi cha 4. Tatizo lililojadiliwa lizalishe mjadala zaidi na kujifunza. Soma maelezo kwenye kitabu cha mshiriki, elezea zoezi, kisha wagawe washiriki katika vikundi vidogo vya watu 5-8 ili kujibu maswali yaliyotolewa. Zoezi hili litahitaji angalau dakika 20-30 kulikamilisha.

Pointi kubwa ya zoezi ni washiriki wafikie kuelewa utata wa maamuzi fulani katika huduma ya kanisa na njia ambazo badiliko moja linaweza kuathiri maeneo mengine mengi ya maisha ya kanisa. Si muhimu sana kutafuta suluhisho la tatizo, lakini cha muhimu zaidi ni washiriki wagundue ugumu wa masuala yaliyomo kwenye kusanyiko, matokeo au athari zenye nguvu kwa kila uamuzi katika maeneo mbalimbali ya maisha ya kanisa.

Mwishoni mwa zoezi, waombe vikundi viwili ama vitatu (kadiri muda uanavyoruhusu) wapate mtu atakayewashirikisha wengine jibu la kundi lake katika moja ya maswali yaliyomo kwenye kitabu na uamuzi ambao kundi lake lingeufanya katika suala hili.

## Ufuatiliaji pamoja na Viongozi wa Kanisa lako:

Zungumzieni jinsi sehemu tofauti za Kanisa lenu zinavyoendelea na ni maeneo yapi unayotaka kuyashughulikia.

- Waruhusu Viongozi wa Kanisa lako waorodheshe kila kitu wanachokijua juu ya watu katika ujirani wenu (mivuto yao, mahitaji, nk).
- Wasaili majirani ili kutafiti zaidi juu yao na mitazamo yao juu ya Kanisa.
- Je, unayaelewa zaidi (vizuri) mazingira yako?
- Je, Viongozi wako wanawasiliana vizuri na kusanyiko (Kanisa?)
- Je, washirika wanazitumia karama zao?
- Je, huduma zinalenga juu ya maono na Misheni ya Kanisa au zinalenga makusudi mengine?.

## **Zoezi** | "Zulia Jekundu"

Miaka ishirini iliyopita, kanisa la "Living Water" (Maji Yaliyo Hai) lilifanya sherehe ya uzinduzi wa jengo la kanisa lenye uwezo wa kubeba watu mia moja. Mmoja wa mashemasi wa wakati huo, Michael Smith, akiwa na umri wa miaka 67, alichangia fedha kwa ajili ya zulia na akapendekeza liwe jekundu, kwani rangi nyekundu ndio rangi aliyopendelea zaidi. Kila mtu alifurahia kitendo cha Michael, ikiwa ni pamoja na familia yake, iliyokuwa na ushawishi mkubwa ndani ya kanisa, na zulia jekundu likanunuliwa.

Sasa, miaka ishirini baadaye, kamati ya ujenzi wa kanisa inafikiria kulibadilisha zulia na kuweka jipya litakaloendana na rangi ya mapazia ya bluu ambayo mshirika mwingine, aitwaye Mariamu amechangia. Wanafikiria kutumia fedha zilizochangwa kwa ajili ya marekebisho ya jengo ili wanunue zulia. Hivi karibuni mshirika mzee sana, Michael alitoa mchango mzuri kwa ajili ya marekebisho na akaomba wanunue zulia jekundu tena. Familia yake wamekubaliana na ombi hili, lakini kamati ya ujenzi wangependa kuweka sakafu maalumu itakayofaa kwa matumizi yote

Mchungaji ameshikwa na wasiwasi. Anajua sana ushawishi wa familia ya Smith, lakini, vilevile amewapa mamlaka kamati ya ujenzi kufanya mabadiliko na kufanya mabadiliko ya ambalo litafaa kwa matumizi mbalimbali. Ingawa hawezi kuamini kwamba watu wanaelekea kubishana juu ya kitu kisicho na maana wakati yapo mahitaji mengi katika jamii,kuna watu kadhaa kutoka kila kundi wametishia kuhama kanisa kama maamuzi hayataendana na wanavyotaka:

a. Ndugu yake na Michael ambaye hajahudhuria Ibada muda mrefu alisema hawezi kabisa kurudi tena Kanisani ikiwa kamati haijali/haitaheshimu zawadi na matakwa ya Michael.

b. Mshirika wa muda mrefu wa Huduma ya wanawake ambaye amekuwa akiwahubiri watu kwenye jamii alisema, ikiwa kamati itakubaliana na matakwa ya mtu mmoja juu ya mahitaji ya Huduma za Kanisa, atatafuta (atahamia) Kanisa lingine.

c. Familia kadhaa zenye vijana wadogo zimesema kwamba Kanisa linahitaji kuangalia zaidi huduma yake kwa watoto.

Utata zaidi ni kwamba hivi karibuni Michael Smith amekuwa mgonjwa na amefanyiwa upasuaji wa moyo.

Kamati imemwalika Mchungaji kwenye kikao chao cha jioni ili kujadili juu ya hali hii.

Kwenye makundi ya watu 3 – 5, jifikirieni kwamba ninyi ndio kamati na mnakutana na Mchungaji ili kujadili hali hiyo. Tumieni maswali haya ili yawasaidie kutafakari na kuleta mapendekezo:

1. Je, hali hii ndani ya Kanisa ina athari kwenye jamii? kwa namna gani?

2. Je, hali hii inayaathiri maeneo yoyote ya Kanisa kati ya yaliyoorodheshwa hapa chini? kwa vipi?

| | | |
|---|---|---|
| Mahali | Uongozi | Historia ya shirika |
| Maono/kusudi | Washirika | Maadili ya Kanisa |
| Rasilimali | Muundo | Maeneo mengine |
| Mipango | Mazingira/Mawasiliano | |

3. Je, Kanisa lina uchaguzi upi? Je, kuna uwezekano wa matokeo gani kwa kila uchaguzi?

4. Ni kwa namna gani Kanisa linaweza kufanya uwamuzi huu unaoenda na maono na Misheni yake wakati huohuo likiuzingatia mfumo mzima?

**Hitimisho |** Mwishoni mwa warsha:

1. Washiriki wajaze fomu ya tathmini.
2. Ikiwezekana piga picha warsha yako ili kutuma kwa mtandao wa kuzidisha.
3. Watie moyo washiriki kuendeleza hatua na maendeleo ya kanisa lenye afya zilizotolewa na mtandao wa kuzidisha:
   - Hatua inayofuata kwa kanisa baada ya warsha ya kuimarisha kanisa lako ni kufanya somo la kibinafsi juu ya vidokezo maalum na kazi za kanisa lenye afya yaani "Pima Mshipa wa Kanisa Lako" Angalia tovuti ya mtandao wa kuzidisha au wasiliana na mwakilishi kwa taarifa juu ya suala hili.
   - Makanisa yanayojihusisha au yanayovutiwa na upandaji wa kanisa yanaweza kuhitaji kushiriki katika mpango wa "Makanisa mengi zaidi".
   - Fungeni kwa maombi.

**Maelezo kwa mnenaji wa kanisa la mahali pamoja |** Katika ukurasa wa kitabu cha mshiriki utapata hatua za msingi za kufuata ikiwa mchungaji au kiongozi angependa kufanya kongamano hili katika kanisa lako la mahali pamoja au dhehebu lake. Vile vile utapata maelezo juu ya ripoti ya kutuma kwa mtandao wa kuzidisha.

Tafadhali endelea kuchunguza watu watakaoweza kuongeza warsha hii kwa wakati ujao. Ni muhimu viongozi watafute njia za kuzidisha timu zao za wanenaji zenye wakufunzi wa ubora wa hali ya juu kwa warsha zijazo

**Tathmini |** Kila warsha itapaswa kuhitimishwa kwa washiriki kujaza karatasi ya tathmini. Baada ya kupitia maoni ya washiriki tafadhali tuma karatasi hizi ( au muhtasari wa majibu) kwa mwakilishi wa mtandao wa kuzidisha aliye karibu nawe au jaza fomu ya ripoti kupitia tovuti yetu ya www.multiplicationnetwork.org

**Vyeti |** Warsha nyingi zinahitimishwa kwa kukabidhi vyeti vya ushiriki. Ukipenda unaweza kutoa nakala ya cheti hiki au kuunda kinachofanana kwa kutumia msemo wa kanisa lililofadhili warsha yako.

## KUHITIMISHA WARSHA

Kanisa linaloleta tofauti:

1. Linatii Amri Kuu (Mt 22:37)
    - Mpende Bwana Mungu kwa moyo wako wote.
    - Mpende jirani yako kama nafsi yako.
2. Hutimiza Agizo kuu (Mt 28:18-20)
    - Enendeni mkawafanye wanafunzi .
    - Mkiwabatiza.
    - Kuwafundisha kuyashika yote aliyofundisha Yesu.

Kila Kanisa limeitwa kukua katika upendo wake kwa Mungu, kwa wengine ndani ya familia ya Mungu, na kwa wale wanaohitaji kumjua Mungu. Kanisa linaloleta tofauti linaelewa kwamba Misheni kamilifu ndilo kusudi lake na hufanya ufuatiliaji kwa waumini.

Moja ya Makanisa yanayokua kwa kasi zaidi ulimwenguni lilitoa msemo huu:

***"KUJITOA KWA NAMNA KUU katika AMRI KUU NA AGIZO KUU hufanya KANISA KUU."***

# KIAMBATANISHO | MISINGI YA KITHEOLOJIA

Stuart Murray anafupisha misingi ya Kitheolojia kwenye kitabu chake kiitwacho "Kuweka Misingi" Vyote yaani kukua kwa Kanisa na kupanda Makanisa mapya vina misingi katika kanuni tatu.

1. **KUVAA MWILI.**
   Kwa njia ile ile ambayo Mungu alivaa mwili katika Yesu ili kujihusisha na ubinadamu, Kanisa linapaswa kuvaa mwili katika jamii fulani na mahitaji yake nakuleta ujumbe wa Injili kamili. Kanisa ni mwili wa Kristo ulio mahali fulani, ukijihusisha na watu ili kuwafikia kwa habari njema za uzima katika Kristo

   **Mistari ya ufunguo** | Fil. 2:5 – 8
   Yn. 1:1, 1-14

   *"Katika historia yote kumekuwa na wanadamu wengi ambao wametamani kuwa kama miungu, lakini ni Mungu mmoja tu aliyewahi kuwa mwanadamu"*

2. **MISSIO DEI: " MISHENI YA MUNGU"**
   Mungu wa Biblia ni Mungu ambaye siku zote huwatafuta waliopotea na wahitaji ili kuwaletea wokovu na mabadiliko. Vivyo hivyo, kanisa linapaswa kumfuata Mungu katika agizo lake la kufanya wanafunzi, kubadilisha jamii na kuwa wakala wa mabadiliko kwa niaba ya Mungu pamoja na Mungu katika shughuli yake ambayo tayari inaendelea ulimwenguni.

   **Mistari ya Ufunguo** | Yn. 3:16
   Mt. 28:18-20, Mk. 16:15-16, Lk. 24:46-49

   *"Kanisa lipo kwa misheni kama moto ulivyo kwa kuunguza."*
   *-Emil Brunner*

3. **UFALME WA MUNGU**
   Kanisa linatangaza na kuonesha yale aliyotangaza Yesu na kuyaonesha – kuja kwa ufalme wa Mungu! Kanisa linapoonesha linafanyika mwili na kufundisha wema wa Mungu, utawala wa Mwenyezi juu, uumbaji na viumbe vyake

   **Mistari ya Ufunguo** | 1Pet. 2:9-12,
   Kol. 1:13

   *"Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu na mengine yote mtazidishiwa." -Yesu Kristo (Mt. 6:33)*

**MAONI |**

## FOMU YA TATHIMINI |

1. **Je, ungeitathiminije warsha hii ya Kuimarisha Kanisa Lako?**

   ☐ Bora sana ☐ Nzuri sana ☐ Nzuri ☐ Ya wastani ☐ Mbaya

2. **Je, ungependa kuipendekeza warsha hii kwa mtu mwingine pia?**

   ☐ Ndiyo ☐ Inawezekana ☐ Sidhani ☐ Hapana

3. **Je, ungependa kuongezea kitu gani katika warsha hii?**

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

4. **Je, ungependa kuondoa kitu gani katika warsha hii?**

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

5. **Je, unatathiminije maandalizi ya viongozi wa warsha?**

   ☐ Bora sana ☐ Mazuri sana ☐ Mazuri ☐ Ya wastani ☐ Mabaya

6. **Je, michoro ilikusaidia kukielewa kipindi?**

   ☐ Ilinisaidia sana ☐ Ilinisaidia kidogo ☐ Haikunisaidia sana ☐ Haikunisadia

7. **Zungishia namba inayoonesha maoni yako juu ya kipindi:**

| | KIWAN-GO CHA JUU | | | | KIWANGO CHA CHINI |
|---|---|---|---|---|---|
| KIPINDI CHA 1 \| Shauku, Maono, Dhamira | 5 | 4 | 3 | 2 | 1 |
| KIPINDI CHA 2 \| Ishara Tano za Kanisa Lenye Afya | 5 | 4 | 3 | 2 | 1 |
| KIPINDI CHA 3 \| Kazi Tano za Kanisa Lenye Afya | 5 | 4 | 3 | 2 | 1 |
| KIPINDI CHA 4 \| Mfumo wa Mabadiliko | 5 | 4 | 3 | 2 | 1 |

8. Maoni mengine au ushauri:

   ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

**WARSHA ZIJAZO |**

Ikiwa wewe ni Mchungaji au kiongozi wa Kikristo na ungependa kongamano hili liendeshwe katika kanisa lako la mahali pamoja au ungependa kushiriki kama mnenaji wa kongamano, unaweza kufanya yafuatayo:

1. Andaanakuongozawarshayaukuajimkamilifuwakanisakwakutumia vitabu vya mwongozo vya washiriki na viongozi vinavyopatikana bure kupitia mtandao wa www.multiplicationnetwork.org.

2. Wasiliana na mwakilishi wa mtandao wa kuzidisha na umuombe akusaidie kuongoza mafunzo katika kanisa lako au kikundi chako.

3. Baada ya warsha, tafadhali tutumie taarifa na picha ya kikundi ulichokifunza. Tafadhali tutumie pia muhtasari wa tathmini. Fomu ya ripoti inapatikana kwa nafasi yako katika mtandao wetu, au unaweza kututumia taarifa zifuatazo:

   - Ripoti ya Tukio la Mafunzo
   - Warsha: Kuimarisha Kanisa lako
   - Jina la Kanisa
   - Anuani ya Kanisa
   - Jina la Mchungaji
   - Jina /Majina ya mtu/watu walioongoza mafunzo
   - Idadi ya washiriki waliopata mafunzo
   - Maoni au ushuhuda mfupi
   - Muhtasari wa tathmini

Siku zote tuwatafute wanenaji wapya ili KUIZIDISHA huduma hii.

Kama unahisi kwamba Mungu anaweza kukutumia kwa njia hii, tafadhali wasiliana nasi kupitia www.multiplicationnetwork.org

red de
multiplicación

*más iglesias, mejores iglesias*

# *Cheti cha Kutambuliwa*

Kwa kumaliza Warsha ya

KUPANDA MAKANISA YENYE AFYA

## KUWA KANISA LENYE MATOKEO!

Iliyofadhiliwa na:

Kimetolewa kwa : ____________________

Mahali: ____________ Tarehe: ____________

*Kuwafunza viongozi kwa ajili ya Ukuaji wa Kanisa na U pandaji ea Kanisa*
www.multiplicationnetwork.org